

# CHUO CHA KUMBUKUMBU YA MWALIMU NYERERE



## MAHAFALI YA KUMI NA TATU (13) KIVUKONI KAMPASI NA MAHAFALI YA TATU (3) ZANZIBAR KAMPASI - 2018

Mkuu wa Chuo anawatangazia wanafunzi waliohitimu masomo yao katika mwaka wa masomo 2017/2018 kwamba **Mahafali ya Kumi na Tatu** yatafanyika kwenye Kampasi ya Kivukoni, **Ijumaa tarehe 30 Novemba, 2018** kuanzia saa **4:00** asubuhi na **Mahafali ya Tatu** katika Kampasi ya Zanzibar yatafanyika **Jumatatu tarehe 3 Disemba, 2018** kuanzia saa **4:00**

### Wahitimu wanatakiwa kuzingatia yafuatayo:

1. Kuthibitisha ushiriki wao katika Ofisi ya Udahili kabla ya **tarehe 28 Novemba, 2018** kwa Kampasi ya Kivukoni na kabla ya **tarehe 30 Novemba, 2018** kwa Kampasi ya Zanzibar.
2. Kuchukua Majoho kwenye ofisi namba 115 – Jengo la Uhuru **Kampasi ya Kivukoni** kuanzia **Jumatatu, tarehe 26** hadi **Alhamis, tarehe 29 Novemba, 2018** wakati wa saa za kazi na kwa **Kampasi ya Zanzibar** wafike Ofisi ya PMU kuanzia **Jumatatu tarehe 26** hadi **Ijumaa tarehe 30 Novemba, 2018** kuanzia saa 4:00 asubuhi hadi saa 9:00 alasiri. **Majoho hayatatolewa siku ya mahafali.**
3. Kila mhitimu anatakiwa kulipa **shilingi 40,000/=** kwa ajili ya kukodi joho na fedha hizo hazitarejeshwa. Kwa Kampasi ya Kivukoni, malipo yafanyike CRDB Bank Ltd, Akaunti Namba 015206210001, Jina la Akaunti ni **“MNMA-DSM Operation”**, na kwa **Kampasi ya Zanzibar**, malipo yafanyike CRDB Bank Ltd, Akaunti Namba 0150416197400, Jina la Akaunti ni **“ The Mwalimu Nyerere Memorial Academy Zanzibar.**
4. Majoho sharti yarejeshwe Chuoni kabla ya **tarehe 7 Disemba, 2018** kwa **Kampasi ya Kivukoni na Kampasi ya Zanzibar..** Vinginevyo faini ya **shilingi 10,000/=** itatozwa kwa siku kwa yeyote atakayechelewa kurudisha joho.
5. Zoezi la namna ya kupokea vyeti (**rehearsal**) litafanyika **Alhamis, tarehe 29 Novemba, 2018** kuanzia saa **6.00 mchana** katika uwanja wa Mahafali **Kampasi ya Kivukoni na Kampasi ya Zanzibar** zoezi hilo litafanyika **Jumapili tarehe 2 Disemba, 2018** kuanzia saa **4:00 asubuhi** katika uwanja wa mahafali.. **Mhitimu atakayeshindwa kuhudhuria zoezi hilo, hataruhusiwa kushiriki katika Mahafali hayo.**
6. Kila mhitimu atapaswa kujigharamia usafiri, malazi na chakula.

Nyote Mnakaribishwa.

Mkuu wa Chuo,  
Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere,  
S.L.P. 9193,

**DAR ES SALAAM.**

Simu: +255 22 2820041/ 2820045/ 2820047

Faksi: +255 22 2820816

Barua pepe: [rector@mnma.ac.tz](mailto:rector@mnma.ac.tz)